

SURA YA KWANZA

KWANINI UNAHISI KUOGOPA KIFO?

Mwaanadamu wengi anaogopa kifo kuliko kitu chochote kile, lakini kinachomfanya kuwa na hofu kuhusu kifo sio mazingira ambayo wengi wanaweza kujiuliza itakuwaje huko?

Nini kinatokea mala baada ya kufa n.k. ukiutazama mfumo wa mawazo hayo yote yanakupa taswira kuwa wanadamu wengi bado hawana uhakika na vile wanavyoishi leo yao katika maisha ya kila kisu.

Wengine wanaogopa kufa wakihofia pengine yale waliyo yaanzisha kweli yata dumu? Bilashaka hao niwale ambao imani zao zimeshikamana katika vitu. Tajiri anawaza akifa (**ideals**) yani mawazo au mipango aliyopanga kuifanya miaka 10 ijayo itafanikiwa nivizuri watu kufikilia endapo wataondoka bila yakuona dira ya mambo wayatarajiayo au wanayofanya itakuwaje hofu nyingi ziko kwenye mali mawazo na nini kitatokea mala baada yakufa.

Unajuwa kile mungu alichokuleta ufanye duniani?

Hakuna mwanadamu aliyezaliwa kwa bahati mbaya kwanza neno bahati mbaya niusemi wa watu ambao hawana imani na ambao wanaamini kwenye suala zima la bahati,

kuamini katika bahati nisawa nakucheza mchezo wa bahatina sibu mungu hana bahatinasibu kwenye uumbaji wa mwanadamu au mtu au kitu mungu hana hayo wala hana farisafa hiyo.

Ikiwa tunamaini yakuwa kila mtu aliyeumbwa nakuja duniani kuna kitu amekuja kukikamilisha je imekupasa kujiuliza unafahamu umekuja kwa kazi gani kwenye ulimwengu huu?

Kama hujui nilazima utaogopa kifo hofu yako katika kifo itakuwa kubwa sana maisha yako pia yanakuwa magumu sio kwa nje ya watu tu, bali hata ndani yako maisha yatakuwa magumu nazuwa pengine inaweza kuwa vigumu kuelewa maisha ya nje naya ndani ni yapi?

Watu wanaweza kuona ugumu kwako lakini wewe katika uhalisia wa kweli kwa jinsi unavyo jielewa kutokana nakulijuwa kusudi lako unaona kabisa maisha yanaenda haijalishi hata kama wengine hawaoni.

Lakini endapo na ndani hauko vizuri hujui kusudi lako unaishi kwa tafsiri yakuona umezaliwa bahati mbaya huko ndiko kuwa na ugumu mpaka ndani na hapo ukiwa hivyo kuwa na hofu kubwa kuhusu kifo nijambo lakufikia kama unalijuwa kusudi lako kwanini uogope kifo bala yaku hofia dhambi?

Hofu juu ya kifo ni moja ya kiashirio kuwa mtu aishi kulingana na maelekezo ya mungu ikiwa uishi kutokana na maelekezo ya mungu hofu juu ya kifo itakuwa kubwa kwako,

Mwovu shetani anatuonyesha kifo kama sababu ya kuhofia yakuweweseka wakati kimsingi kifo sio kitu chakumfanya mtu ahofu kiasi hicho ikiwa unatenda na kuenenda katika mungu kwa mazuri anayo kuasa kwanini uogope kifo? Kifo kina tafasiri kuu mbili.

Umemaliza kazi yako mungu aliyokuumbia hapa duniani au umekufa kwa sababu ya Yule mwovu anaye wajaribu watu usiku namchana. Yani kuna umauti

wa nuru na umauti wa giza kama jinsi ilivyo imani kuna imani aina mbili imani ya mungu na imani ya miungu (mizimu) ikiwemo kufanya matambiko n.k.

Maana yake kama humwamini mungu nilazima utakuwa kwenye upande mwengine wa kuamini imani nyingine hakuna mwanadamu mwenye imani mbili nilazima atakuwa na kilicho mjaa kati ya kimoja wapo.